KISWAHILI · SWAHILI

# Nyenzo kwa ajili ya Jamii Jimbo la New York

Mwongozo wa Rasilimali na Taarifa
kwa wahamiaji New York
Septemba / Oktoba 2025





**New York Immigration Coalition**
nyic.org

Shirikisho la Wahamiaji New York wameandaa nyenzo hii ili kuwasaidia wanajamii, wadau wetu na wanaofanya kazi pamoja nao. Nyenzo hii inaboreshwa mara kwa mara kwa kutegemeana na mabadiliko ya sera na sheria.

Taarifa ilisasishwa mara ya mwisho: 10.28.2025

## Yaliyomo


- Afya **3**
- Habari za sera za uhamiaji **5**
- Taarifa na Rasilimali kuhusu Kuwekwa Kizuizini **8**
- Rasilimali kwa ajili ya familia **9**
- Shule na elimu **10**
- Uwezeshwaji wa Kiuchumi **11**
- Demokrasia **12**
- Fahamu Haki Zako **13**
- Usalama wa Jamii **14**
- Taarifa zinazopatikana NYS **15**

# Afya




**Bima ya afya**

- Wakazi wa New York wanaweza kupata bima ya afya ya umma na bima ya afya ya kampuni binafsi kupitia NY State of Health.
  - Ukikidhi vigezo kwa kuwa na Medicaid, Essential Plan au Child Health Plus, kipindi cha kujiandikisha kiko wazi mwaka mzima.
  - Kipindi cha kujiandikisha kwa bima ya afya ya kampuni binafsi kimeshakwisha.
    - Kipindi cha kujiandikisha ni kuanzia Novemba 1 hadi Januari 15.
- Jinsi ya Kujiandikisha
  - Pata msaada wa bure wakati wa kujiandikisha kutoka kwa Navigator, ana kwa ana au kupitia simu. Tafuta Navigator hapa: info.nystateofhealth.ny.gov/ipanavigatorsitelocations
  - Pigia simu Kituo cha Kuwahudumia Wateja cha NY State of Health 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220).
  - Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov. Kipengele cha ku-chat kinapatikana kwenye tovuti wakati wa masaa ya biashara kwa ajili ya kukusaidia kukamilisha fomu yako ya maombi.
  - Wakazi wa New York City: piga 311, tuma SMS inayosema "CoveredNYC" kwenda 877-877, au tembelea on.nyc.gov/healthinsurance kwa msaada na taarifa zaidi.
- Pata taarifa kuhusu mafao ya bima ya afya kwa lugha mbalimbali hapa: info.nystateofhealth.ny.gov/InformationalMaterials

**Sheria ya Mswada Mmoja Mzuri Sana (One Big Beautiful Bill Act [OBBBA])**

- Hivi karibuni serikali ya shirikisho ilipitisha Sheria ya Mswada Mmoja Mzuri Sana (One Big Beautiful Bill Act [OBBBA])
- Inawezekana kwamba Sheria ya OBBBA itaathiri Medicaid na Essential Plan, lakini hadi sasa bado hakuna mabadiliko. Vigezo na mafao ni vilevile.
- Kupata taarifa za kisasa, tembelea info.nystateofhealth.ny.gov/stay-connected

**Mabadiliko ya Mafao ya Bima ya Afya kwa Wanaopokea DACA**

- Kuanzia Agosti 31, 2025, wanaopokea DACA watakuwa hawakidhi vigezo tena kwa mipango ya bima ya afya ya Sheria ya Huduma Nafuu ya Afya (Affordable Care Act [ACA])
- Hakuna mabadiliko ya kukidhi vigezo vya mipango mingine, mfano Essential Plan au Qualified Health Plans.
- Kwa taarifa zaidi kuhusu mafao ya bima ya afya kwa wanaopokea DACA, tembelea nilc.org/resources/affordable-care-act-for-daca-recipients-a-guide-to-apply
- Inawezekana kwamba hivi karibuni kutakuwa na mabadiliko mengine ya mafao ya bima ya afya kwa wanaopokea DACA. Kufuata habari zote za mabadiliko haya, angalia healthcare.gov.

**Mafao ya Medicaid kwa Wahamiaji Wasio na Vibali katika Jimbo la New York**

- Wahamiaji wasio na vibali wanaoishi katika Jimbo la New York, kuwa na umri wa miaka 65 au zaidi, na kukidhi vigezo fulani vya mapato, wamekidhi vigezo vya mafao kamili ya Medicaid (tofauti na mafao ya dharura tu ya Medicaid)
- Watoto wasio na vibali vya makazi wenye umri wa chini ya miaka 19 wamekidhi vigezo vya mpango wa Child Health Plus (CHP), ambao unatoa mafao ya bima ya afya kwa bure au kwa bei ndogo, bila kujali mapato wala hali ya uhamiaji.
- Medicaid haihesabiwi kama 'public charge,' yaani kuwa wajibu wa serikali, na haiathiri uwezo wa kukidhi vigezo vya kupata kadi ya kijani (green card).
- Jinsi ya kujiandikisha
  - Ikiwa una Medicaid ya Dharura sasa hivi, unaweza kuhamia Medicaid ya kawaida kwa kufuata maelekezo uliyopewa kwenye barua kutoka NY State of Health.
    - Unaweza pia kuchagua kuendelea kupokea Medicaid ya dharura tu.
  - Kama huna bima ya afya, na bado hujapokea Medicaid ya Dharura, unapaswa kutuma maombi kupitia Idara ya Huduma za Jamii (DSS) au kupitia Utawala wa Rasilimali Watu New York (HRA).
  - Ukihitaji msaada au ukiwa na maswali, piga simu NY State of Health 1-855-355-5777. Huduma ya tafsiri inapatikana.

**Vipimo vya Kansa/Saratani**

- Vipimo vya kansa/saratani vinavyofuata mpango vinasaidia kugundua kansa/saratani mapema, inapokuwa rahisi zaidi kutibia.
- Mipango mingi ya bima ya afya inajumuisha vipimo vya kansa/saratani.
- Ikiwa huna bima ya afya, Jimbo la New York inatoa vipimo vya kansa/saratani vya bure kwa kansa/saratani ya matiti, shingo ya kizazi, na utumbo mpana na rektamu.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea health.ny.gov/diseases/cancer/services

# Afya



**Chanjo salama na za kufaa za UVIKO-19, Mafua na RSV zinapatikana**

- Chanjo ni kifaa chenye nguvu kubwa sana kukinga afya na kuzuia maradhi makali. Chanzo zinafanyiwa utafiti na uangalizi kwa umakini, na zinashauriwa na wataalamu wa kitabibu wanaoaminika.
- Unaweza kutegemea vyanzo vya taarifa vinavyoaminika, mfano Kituo cha Kudhibiti Maradhi (Centers for Disease Control and Prevention [CDC]), Idara ya Afya ya Jimbo la New York, au daktari wako, ili ufanye maamuzi mazuri kwa ajili yako na kwa ajili ya familia.
- Chanjo Mpya ya UVIKO-19 ya 2025-2026 inapatikana sana.
  - Chanjo Mpya ya UVIKO-19 inafaa kwa aina nyingi za kirusi zinazoonekana jimboni New York na Marekani nzima.
  - Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani (Food and Drug Administration [FDA]) inashauri kwamba watu wazima wenye umri wa miaka 65 na zaidi, pamoja na watu wenye umri wa miaka 12-64 ambao wanaathirika na maradhi, wapigwe sindano ya booster (kiongeza nguvu).
  - Kwa taarifa zaidi kuhusu chanjo ya UVIKO-19 ya 2025-2026, tembelea cdc.gov/covid/vaccines
  - Kupata chanjo mpya katika kituo ambacho kiko hapo karibu, tembelea vaccines.gov
  - Ukiwa na dalili za UVIKO-19 au ikiwa umekuwa karibu na mtu mwenye UVIKO-19, nenda kapime.
    - Upimaji wa UVIKO-19 unaweza kukusaidia kufanya maamuzi ukiwa mgonjwa, kuhusu kupata matibabu ya awali ili kuzuia maradhi makali, au kujitenga ili kupunguza hatari ya kuwaambukiza watu wengine.
- Chanjo mpya ya mafua, ya mwaka 2025-2026, itapatikana kuanzia Fall 2025.
  - Chanjo mpya ya mafua inalinda dhidi ya aina tatu tofauti za mafua.
  - Wakala ya CDC inashauri watu wote wenye umri wa miezi sita au zaidi wapate chanjo ya mafua.
  - Watu wenye umri wa miaka 65 au zaidi, watu wenye maradhi fulani ya kuselelea, watoto wachanga, na wanawake wajawazito wako kwenye hatari kubwa zaidi ya kuwa na matatizo mazito kutokana na mafua.
- Chanjo ya Kirusi cha Mfumo wa upumuaji cha Sinkitio [RSV] inapatikana sasa.
  - Chanjo inaweza kusaidia kuzuia magonjwa ya mfumo wa upumuaji yanayosababishwa na RSV, hasa kwenye sehemu za chini za mfumo wa upumuaji.
  - Chanjo inashauriwa kutegemeana na umri wa mtu na hali zingine zinazoweza kumweka mtu hatarini.
    - Watu wenye umri wa miaka 75 au zaidi wanashauriwa kupata chanjo.
    - Watu wenye umri wa kati ya miaka 50 na 74 afadhali wazungumze na madaktari wao (au wanaowatolea huduma za afya) kugundua kama wako kwenye hatari ya kuathirika vibaya na RSV.
    - Wanawake wajawazito wanaweza kuwalinda watoto wao kutoka RSV kupitia chanjo ya akina mama. Wanawake wajawazito afadhali wawasiliane na madaktari yao ya uzazi/jinakolojia kupata taarifa zaidi.
  - Vilevile kuna dawa za kuzuia RSV kwa ajili ya watoto wachanga na waliozaliwa hivi karibuni. Dawa hizi zinaitwa nirsevamab na clesrovimab.

**Mlipuko wa Ugonjwa wa Surua na Chanjo ya Surua**

- Kumekuwa na milipuko mingi ya surua hivi karibuni. Surua ni ambukizo la kirusi ambalo ni hatari kubwa kwa watoto wadogo.
- Chanjo ya surua, matumbwitumbwi, na rubela [MMR] inafaa sana kwa kuzuia surua.
  - Chanjo ya MMR inapewa kwa dozi mbili. Dozi ya kwanza inapewa mtoto akiwa na umri wa miezi 12-15, na dozi ya pili inapewa mtoto akiwa na umri wa miaka 4-6.
  - Watoto, vijana na watu wazima ambao hawakupata chanjo ya MMR kwa wakati wanaweza kuipata kwa ratiba maalumu, maanake kupata dozi ya kwanza halafu kuifuata na dozi ya pili wiki 4 badaaye.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea cdc.gov/measles

**Chanjo ya HPV**

- HPV ni kirusi kinachoweza kuenea kupitia watu wagusiane ngozi kwa ngozi. HPV inaweza kusababisha kansa/saratani kama kansa/saratani ya shingo ya kizazi na kansa/saratani ya koo.
- Chanjo ya HPV inashauriwa kwa watu wote chini ya umri wa miaka 26.
  - Inashuriwa kwamba watoto wenye umri wa miaka 11-12 wapate dozi mbili. Dozi ya pili ipewe miezi 6-12 baada ya dozi ya kwanza.
  - Watu wenye umri wa miaka 15-26 wapate dozi tatu. Dozi zipewe ndani ya kipindi cha miezi 6.
- Watu wenye umri mkubwa zaidi kuliko miaka 27 washauriane na wanaowatolea huduma za afya.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea cdc.gov/hpv/vaccines

# Habari za sera za uhamiaji



**Ada Mpya za Uhamiaji**

- Baada ya mswada wa serikali ya shirikisho wa kodi na matumizi wa fedha ulisainiwa ili uwe sheria, ada nyingi za kutuma maombi ya uhamiaji zimebadilika au kuongezeka.
- Baadhi ya nyongeza hizi zinaanza Julai 22, 2025, na zingine zinaanza Agosti 21, 2025.
- Vilevile sera za kusamehewa ada zimezuiwa katika baadhi ya michakato ya kutuma maombi.
- Mabadiliko yanayoweza kuwaathiri wanaotuma maombi ni:
  - Ombi la Hifadhi (Asylum)
    - Ada iliopita: $0
    - Ada Mpya: $100
    - Pia kuna ada mpya ya kila mwaka jina lake 'asylum maintenance fee' yaani ada ya matengenezo ya hali ya hifadhi.
    - Haiwezekani kusamehewa ada hii.
  - Nyaraka za Ruhusa ya Kufanya Kazi (Employment Authorization Documents [EAD]) / Vibali vya Kazi vinavyohusika na Hifadhi
    - Ada iliopita: $0
    - Ada Mpya: $550 (kwa wanaotuma maombi kwa mara ya kwanza)
    - Ada Mpya: $275 kwa kufufua
  - Hali ya Kulindwa kwa Muda (Temporary Protected Status [TPS])
    - Ada iliyopita: $50
    - Ada Mpya: $550
  - Mhamiaji Kijana Maalumu (Special Immigrant Juvenile [SIJ])
    - Ada iliyopita: $0
    - Ada Mpya: $250
  - Parole (msamaha wa muda dhidi ya kuondolewa)
    - Ada Iliyopita: Mbalimbali
    - Ada Mpya ya Ziada: $1,000
    - Hii ada mpya ya ziada ni kwa watu ambao wamepewa hali ya parole na wanakuwepo Marekani sasa hivi.
    - Utalipia ada hii ya ziada ikiwa tu ombi lako la parole linakubaliwa. Usilipie ada ya ziada wakati wa kuwasilisha fomu I-131.
- Kwa orodha nzima ya ada za uhamiaji, na kuzilinganisha na ada zilizokuwepo kabla, utembelee immigrantjustice.org/research/explainer-trump-and-congresss-punishing-new-immigration-fees


**Marufuku ya Safari**

- Juni 9, Utawala wa Trump ulitekeleza marufuku ya safari inayozuia kusafiri Marekani kwa watu kutoka kwa nchi 19.
- Kuna marufuku kamili kwa nchi za Afuganistani, Chadi, Jamhuri ya Kongo, Ginekweta, Eritrea, Haiti, Irani, Libya, Somalia, Sudani, na Yemen.
- Kuna marufuku isiyo kamili kwa nchi za Burundi, Cuba, Laosi, Siera Leoni, Togo, Turukimenistani, na Venezuela.
- Marufuku inajumuisha watu wote kutoka nchi hizi wakiwa nje ya Marekani. Inazuia watu kutoka nchi hizi wasiingie Marekani pamoja na kuzuia wasifufue viza na wasiongeze muda wa viza vilevile.
  - Marufuku isiyo kamili inaondoa uwezo wa kupata viza za biashara, utalii, na viza ambazo msingi wake ni uhusiano wa kifamilia.
  - Marufuku kamili inaondoa uwezo wa kupata viza za biashara, utalii, na viza ambazo msingi wake ni uhusiano wa kifamilia, pamoja na viza zinazoweza kukufikishia kibali cha makazi, maarufu "viza za wahamiaji."
- Marufuku haijumuishi watu ambao tayari wana vibali vya makazi (green card), baadhi ya visa ambazo msingi wake ni uhusiano wa karibu wa kifamilia, na Waafugani wenye viza maalumu za wahamiaji (Special Immigrant Visas).
- Ikiwa unatoka mojawapo ya nchi hizi na una wasiwasi kuhusu viza yako, uzungumze na mwanasheria.

**CBP One Parole na Parole kwa watu wa Cuba, Wahaiti, Wanikaragua, na Wavenezuela (CHNV)**

- Serikali ilituma matangazo yaliyokusudia kufuta hali ya parole ya watu walioingia Marekani:
  - Kupitia miadi ya CBP One; na
  - Chini ya programu ya parole ya Cuba, Haiti, Nikaragua, na Venezuela (CHNV).
- DHS iliwatumia matangazo watu wenye hali ya parole kupitia barua pepe, posta, au kwa kutumia app.
- Ikiwa uliingia Marekani kwa kutumia CBP One au CNHV, na hujatuma maombi kwa manufaa mengine yoyote ya uhamiaji:
  - Hali yako ya parole na kibali chako cha kazi siyo halali tena.
  - Inawezekana kwamba utawekwa kizuizini na kuondolewa nchini kwa nguvu.
- Ikiwa umetuma maombi kwa USCIS kwa manufaa mengine ya uhamiaji, mfano hifadhi, inawezekana kwamba utaweza kuendelea kutafuta manufaa hayo. Pia inawezekana kwamba utakidhi vigezo vya kupata kibali cha kazi kupitia manufaa hayo.
- Ikiwa ulipokea tangazo lililosema kwamba hali yako ya parole ilifutwa, ni muhimu uzungumze na mwanasheria wa uhamiaji karibuni iwezekanavyo ili ujue una machaguo gani.

# Habari za sera za uhamiaji



**Hatua Iliyoahirishwa kwa Kuwasili kwa Utotoni (DACA)**

- Sasa hivi, DACA inaamuliwa mahakamani. Inamaanisha kwamba bado hakuna uhakika kuhusu programu hiyo kwa siku za mbele.
    - Kwa taarifa zaidi, tembelea homeishere.us/daca-guidance
- Kwa mujibu wa amuzi la mahakama la hivi karibuni, lililotoka mnamo Machi 12, 2025, kutuma maombi ya DACA kungeruhusiwa kwa watu wayatumao kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, bado hakuna mwongozo mpya kutoka kwa USCIS.
    - Kama unakidhi vigezo vya DACA na unafikiria kutuma maombi kwa mara ya kwanza, uzungumze na mwanasheria wa uhamiaji anayeaminika kabla ya kutuma maombi.
- Kesi hiyo bado iko mahakamani, kwa hiyo inawezekana kuwa kutakuwa na mabadiliko mengine kwenye programu hiyo.
- Kwa sasa, Wizara ya Usalama wa Ndani (DHS) itaendelea kupokea na kujibu maombi ya DACA, pamoja na maombi ya vibali vya kazi na advanced parole (ruhusa ya kuingia Marekani tena ukitoka bila kuwa raia au kuwa na kibali cha makazi). DHS itapokea maombi ya awali ya DACA lakini haitayafanyia kazi kwa sasa.
    - Ikiwa wewe ni mnufaika wa DACA kwa sasa, unufaika wako ni halali.
    - Iwapo haki yako ya kupokea manufaa ya DACA yanaisha ndani ya miezi sita, ifufue tena leo!
    - Kama ulituma maombi ya kujiunga na programu ya DACA kwa USCIS kwa mara ya kwanza na bado hujajibiwa, fahamu kuwa mchakato huo ulisitishwa. Hautaendelea mpaka kipindi ambacho bado hakijafahamika.
- Wanufaika wa Hatua Iliyoahirishwa kwa Kuwasili kwa Utotoni (DACA) wanaweza sasa kujaza Fomu I-821D (maombi ya kufufua DACA) na I-765 (maombi ya kufufua kibali cha kazi) mtandaoni.
    - Maombi ya mtandaoni yanapatikana kwa wale wenye DACA sasa hivi, au wale ambao wamepoteza uanachama wa DACA ndani ya mwaka mmoja uliopita.
    - Kwa taarifa zaidi kuhusu DACA na jinsi ya kufufua hali yako ya DACA, tembelea uscis.gov/DACA

**Hali ya Kulindwa kwa Muda (TPS)**

- Serikali ya Marekani inaweza kuchagua nchi fulani kwa ajili ya kutoa ulinzi wa kipindi kifupi (TPS) ikiwa vigezo fulani kama mapigano au maafa ya asili yanawazuia raia wa nchi hiyo kurejea salama.
- Katika kipindi hicho, watu wanaotuma maombi kwa ajili ya TPS na kupewa watapata yafuatayo:
    - Kutokufukuzwa nchini Marekani
    - Wanaweza kupata vibali vya kazi na namba ya usalama wa kijamii (SSN)
    - Wanaweza kupewa ruhusa ya kusafiri
    - Hawawezi kutiwa nguvuni na DHS kwa sababu ya hali yao ya uhamiaji
- TPS ni manufaa ya muda yasiyopelekea hali ya makazi ya kudumu. Hata hivyo, wenye TPS wanaweza kutuma maombi kwa ajili ya kupokea manufaa mengine yoyote ya wahamiaji au yasiyo ya wahamiaji mradi wawe wanakidhi vigezo.
- Nchi zinazohusika na TPS:
    - Bama (Myama), Esavado, Ethiopia (Uhabeshi), Haiti, Lebanoni, Nikaragua, Somalia, Sudani, Sudani Kusini, Ukraini, Yemen
- Kwa taarifa za nchi mahususi, vigezo vinavyohitajika, tarehe za usajili, na habari zaidi, tembelea uscis.gov/TPS.
- Waombaji wote wa TPS wanaweza sasa kutuma Fomu I-821, Ombi la Hali ya Kulindwa kwa Muda (Application for Temporary Protected Status), mtandaoni katika uscis.gov/i-821.
- Nchi zilizochaguliwa na Wizara ya Usalama wa Ndani (Department of Homeland Security [DHS]) kwa hali ya TPS wakati wa utawala wa Biden zinafanyiwa mapitio. Inawezekana kwamba mapitio haya yanayofanywa na DHS yatakuwa na matokeo ya kufuta hali ya TPS kwa nchi zilizochaguliwa.
    - Februari 1, 2025, DHS ilibatilisha TPS kwa Wavenezuela (kwa njia isiyo kamili).
        - Kukomeshwa kwa Uteuzi wa 2021 wa TPS kwa Wavenezuela kutafanyika Novemba 7, 2025.
    - Agosti 20, DHS iliruhusiwa kukomesha TPS kwa Honduras na Nikaragua, kuanzia Septemba 8.
    - Septemba 22, 2025, DHS ilikomesha TPS kwa Siria, kuanzia Novemba 21, 2025
- Inashauriwa wanajamii waendelee kufuata habari za hali ya TPS ya nchi zao, na kuwa na ujuzi kuhusu hali zao ni zipi.
- Ikiwa hali yako ya TPS inakwisha au imeshakwisha, uzungumze na mwanasheria wa uhamiaji ili ujue una machaguo gani na kuona kama unakidhi vigezo vya programu zingine.

# Habari za sera za uhamiaji

**Kupanuka kwa Kuwaondosha Watu Nchini kwa Haraka (Expedited Removal) Mbali Zaidi na Mpakani**

- Kuanzia Januari 21, Wizara ya Usalama wa Ndani ilipanulisha matumizi yake ya mchakato unaoitwa “expedited removal” (kuwaondosha watu nchini kwa haraka).
- Kabla, ICE na CBP walitumia mchakato wa kuwaondosha watu nchini kwa haraka ikiwa mtu mhusika alikutwa ndani ya maili 100 kutoka mpakani, na ndani ya siku 14 tangu kuingia Marekani.
- Sasa, serikali imetangaza kwamba itatumia mchakato huu wa kuwaondosha watu nchini kwa haraka kumwondosha mtu yeyote asiye na kibali cha makazi ambaye hawezi kuthibitisha kwamba amekuwepo Markeani kwa angalau miaka miwili (bila kutoka na kuingia tena) kabla ya kukamatwa.
- Kuwaondosha watu nchini kwa haraka kunawezesaha serikali kumwondosha mtu ambaye serikali inaamini hana kibali cha makazi, bila kuonekana mbele ya hakimu ya uhamiaji.
- Sasa hivi, kuna njia chache tu za kusamehewa ili usiondolewe nchini kupitia mchakato wa haraka (expedited removal).
    - Njia mojawapo ni kama mtu anadai kwamba anaogopa kurudi nchini kwake, halafu anafaulu mahojiano ya kupima hofu. Hii ingeweza kumruhusu mtu atume maombi ya hifadhi.
- Ni muhimu watu wafahamu haki zao na kufuata hatua za kujilinda na kulinda familia zao, ikiwemo kubeba nyaraka za kuthibitisha kipindi cha makazi cha angalau miaka miwili, ikiwezekana.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea nilc.org/resources/know-your-rights-expedited-removal-expansion/



**ICE katika Mahakama za Uhamiaji**

- Baadhi ya wahamiaji wanaohudhuria usikilizaji wa kesi zao za uhamiaji mahakamani wanawekwa kizuizini na ICE.
- Mahakamani, mwendesha mashtaka wa serikali anaweza kujaribu kufuta kesi yako. Ikiwa miaka miwili bado haijapita tangu ulipofika Marekani, na kesi yako inafutwa, inawezekana kwamba utakuwa hatarini maanake maafisa wa ICE wanaweza kukukamata na kukuondoa nchini kwa haraka. Mchakao huu unaitwa “expedited removal.”
- Jinsi ya kujilinda
    - Ikiwa unaweza, hudhuria usikilizaji wa kesi yako ya uhamiaji kupitia mtandao badala ya kwenda mahakamani penyewe.
    - Ikiwa unakidhi vigezo, hakikisha kwamba umefaili maombi yako ya hifadhi au maombi mengine kwa mahakama.
    - Ikiwa unawekwa kizuizini na unaogopa kurudishwa nchini kwako na/au kupelekwa nchini kengine, sema hii wazi kwa maafisa wa ICE na kwa maafisa wengine wowote wa uhamiaji.
    - Ikiwa maombi yako ya hifadhi yalikuwa mahakamni kesi yako ilipofutwa, haitatosha kukulinda. Lazima ueleze upya hofu yako ya mateso na unyanyasaji.
- Fahamu Haki Zako mahakamani:
    - Una haki ya kupinga ufutaji wa kesi yako kabla hakimu hajafanya maamuzi.
    - Unaweza kudai kwamba mwanasheria wa ICE awasilishe ombi lake la kufuta kesi kwa maandiko, ili uwe na muda wa kumweleza hakimu kwa nini unataka kuendelea na kesi yako na kutafuta msaada wa kisheria.
    - Ikiwa hakimu anafuta kesi yako, una haki ya kukata rufaa. Unaweza kukata rufaa maamuzi hayo kwa Bodi ya Kukata Rufaa za Uhamiaji (Board of Immigration Appeals [BIA]). Uhakikishe kumwambia hakimu ya uhamiaji kwamba unataka kukata rufaa.
    - Ikiwa unaogopa unyanyasaji au mateso ukirudishwa nchini kwako na/au kupelekwa nchini kengine, sema hii kwa hakimu katika usikilizaji.

# Taarifa na Rasilimali kuhusu Kuwekwa Kizuizini

**Jinsi ya kuwa tayari kwa wewe na familia yako**

- Ikiwa wewe si raia wa Marekani na una watoto, uwe na mpango iktokea unawekwa kizuizini na afisa wa ICE, CBP au wakala nyingine.
- Ili kuwa tayari, itabidi ufanye hivi:
  - Tunza vizuri nyaraka muhimu. Uziweke mahali ambapo wanafamilia wengine wataweza kuzipata kama watahitaji.
  - Amua ni nani ambaye ungetaka kuwatunza watoto wako usingeweza kufanya mwenyewe.
  - Umteue kisheria mtu awe mlezi wa watoto wako.
    - Njia mbili kuu za kumteua kisheria mtu awe mlezi ni:
      - Uteuzi wa Mtu katika Uhusiano wa Mzazi (Designation of Person in Parental Relationship)
      - Uteuzi wa Mtu wa Kuwa Mlezi Ikitokea Dharura (Standby Guardianship)
  - Jaza fomu za ziada kwa ajili ya mtoto wako, ikiwemo Travel Authorization Form au School Emergency Contact Form
  - Unaweza kufikiria pia kujaza fomu ya Power of Attorney
  - Kwa taarifa zaidi, tembelea vlpcny.org/get-help/immigration/planning-for-immigrant-parents

**Jinsi ya kuwasiliana na watu ukiwekwa kizuizini**

- Ikiwa unawekwa kizuizini na afisa wa uhamiaji, polisi, au afisa wa chombo kingine cha dola, una haki fulani, ikiwemo haki ya kuwasiliana.
- Una haki ya kupiga simu, mfano kumpigia simu mwanafamilia, mwanasheria au ubalozi.
- Unaweza kupiga simu namba maalumu kwa watu wahamiaji wanaowekwa kizuizini ili upate taarifa zaidi pamoja na rasilimali.
  - Kupiga simu Namba Maalumu ya Kitaifa ya Utetezi wa Wahamiaji, piga 9233# kutoka kwa simu ya mahali ambapo umewekwa kizuizini. Namba maalumu hiyo ni bure, mazungumzo hayasikilikzwi, na huduma zinapatikana Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa tano asubuhi hadi saa tano usiku (11am-11pm).
  - Kupiga simu namba maalumu ya Haki kwa Familia za Wahamiaji (Justice for Migrant Families), inayopatikana kwa wanaowekwa kizuizini Kituo cha Serikali ya Shirikisho cha Buffalo (Buffalo Federal Detention Facility), piga 716-427-4917, Jumatatu hadi Alhamisi, kuanzia saa nane mchana hadi saa kumi mchana (2pm-4pm) na kuanzia saa kumi na mbili jioni hadi saa mbili usiku (6pm-8pm).

**Jinsi ya kumsaidia mtu aliyewekwa kizuizini**

- ICE inaweza kuwaweka kizuizini watu wasio raia katika vituo vinavyoendeshwa na ICE, katika jela, na katika vituo vya kizuizini vinavyoendesha na kampuni binafsi.
- Mfumo wa kizuizini kwa wahamiaji si rahisi kuelewa wala kushughulikia. Kwa sababu hii ni ngumu kumtafuta na kuwasiliana na ndugu yako mpendwa ambaye yuko kizuizini.
- Kumtafuta mtu ambaye yuko kizuizini kwa ICE sasa hivi:
  - Nenda locator.ice.gov na ingiza taarifa zifuatazo:
    - Jina, nchi ya kuzaliwa, na tarehe ya kuzaliwa, au
    - Namba ya “A” (A-number) ya tarakimu tisa
  - Kifaa cha ICE cha kutambua mahali (locator) kinapaswa kuonesha mahali anapowekwa kizuizini mtu mhusika. Lakini inaweza kuchukua muda kabla mtu mhusika hajaonekeana kwenye mfumo.
  - Ukidhani kwamba ndugu yako mpendwa yuko kizuizini kwenye kituo mahususi cha ICE, unaweza pia kumtafuta kupitia:
    - Kumtafuta katika accesscorrections.com. Jina lake likionekana, kuna uwezekano mkubwa kwamba yuko kizuizini kwenye kituo hicho ulichochagua.
    - Kuwasiliana na kituo fulani moja kwa moja kupitia ice.gov/detention-facilities
  - Ikiwa huwezi kumpata mtu mhusika kwa kutumia mifumo hii ya mtandao, unaweza kuwasiliana na ofisi ya ICE aina ya Nyendo za Utekelezaji na Ufukuzaji (Enforcement and Removal Operations [ERO]): ice.gov/contact/field-offices
  - Kwa taarifa zaidi kuhusu kumtafuta mtu ambaye amekamatwa au kuwekwa kizuizini kwa wahamiaji, tembelea nilc.org/resources/how-to-find-a-loved-one-after-a-u-s-immigration-arrest/
    - Rasilimali hii inapatikana katika lugha 9, zikiwemo Kiingereza, Kiarabu, Kichina, Krioli ya Haiti, Kikorea, Kitagalog, Kivietnam na Kihispania.
- Kutafuta tarehe ya kwenda mahakamani, pamoja na mahali:
  - Tembelea acis.eoir.justice.gov na kuingiza namba ya “A” ya tarakimu tisa, au
  - Piga simu 1-800-898-7180 na fuata maelekezo.
- Kupata msaada wa kisheria:
  - Kupata mashirika yasiyo ya faida yanayotoa huduma za kisheria kuhusu uhamiaji, kwa bure au kwa bei nafuu, tembelea immigrationadvocates.org/legaldirectory
  - Piga simu Mradi wa Kuwatetea Wahamiaji (Immigrant Defense Project) katika 212-725-6422
- Kupata msaada wa kulipa dhamana:
  - Ikiwa ndugu yako mpendwa amepewa dhamana asiyoiweza, inawezekana kwamba anaweza kupata msaada kutoka kwa mfuko fulani wa kulipia dhamana.
  - Kwa taarifa kuhusu dhamana katika jimbo la New York, tembelea envisionfreedom.org/get-support
  - Kwa orodha ya mifuko maalumu ya kulipia dhamana katika sehemu mbalimbali nchini, tembelea bit.ly/localbailfunds

# Rasilimali kwa ajili ya familia

**Msaada wa Huduma za Kuangalia Watoto wa Promise NYC**

- Mwezi Januari 2023, Jiji la New York lilizindua Promise NYC, programu mpya itakayotoa msaada wa gharama za kuangalia watoto kwa familia zenye mapato madogo za watoto wasio na vibali vya kuishi Marekani au wasio raia, ambao hawakukidhi vigezo kabla kwa sababu ya kukosa vibali vya uhamiaji.
- Programu imefufuliwa na itawasaidia zaidi ya watoto 1,000 kuanzia Julai 2025 hadi Juni 2026.
- Familia zinaweza kukidhi vigezo ikiwa:
  - Hazikidhi vigezo vya kupata msaada wa programu zingine
  - Zina mtoto mwenye umri wa miaka 0-13
  - Zina mapato ya kaya chini ya 300% ya kiwango cha umasiki cha serikali ya shirikisho
- Familia zinahamasishwa kutuma maombi kwa haraka kwa mashirika ya kijamii yafuatayo yanayohudumia serikali zao za mitaa (borough)
  - Bronx and Manhattan: Northern Manhattan Improvement Corporation (212-822-8300, nmic.org/promisenyc)
  - Brooklyn: Center for Family Life (718-438-9500, centerforfamilylife.org)
  - Staten Island: La Colmena (718-442-7700, lacolmenanyc.org)
  - Queens: Chinese-American Planning Council (718-358-8899, cpc-nyc.org)
- Tafadhali zingatia kwamba nafasi za Promise NYC ni adimu sana, na tunahamasisha familia kujiandikisha kwenye orodha ya wanaosubiri ili ziwe tayari nafasi mpya zikipatikana.



**Programu ya Msaada wa Gharama za Huduma ya Kuangalia Watoto**

- Familia sasa zinakidhi vigezo vya kupata msaada wa gharama za huduma za kuangalia watoto ikiwa mapato yao ni 85% ya wastani wa mapato ya jimbo au chini yake.
  - Familia itakuwa inakidhi vigezo ikiwa na mapato ya mwaka yasiyozidi:
    - $73,896 kwa familia ya watu wawili
    - $91,250 kwa familia ya watu watatu
    - $108,631 kwa familia ya watu wanne
    - $126,012 kwa familia ya watu watano
    - $143,393 kwa familia ya watu sita
  - Gharama haitazidi 1% ya mapato kamili ya familia ambayo yako juu ya kiwango cha umaskini kwa familia zinazoshiriki.
  - Idadi ya siku anazoruhusiwa kukosa huduma kwa kutokuhudhuria kituo cha kuangalia watoto ni siku 80.
- Kwa taarifa zaidi na kuona kama utaweza kupata msaada wa kuangalia watoto kwa gharama ndogo au bila gharama, tembelea ocfs.ny.gov/ccap.

**Mapumziko Yaliyolipiwa kwa ajili ya Mama Wajawazito katika Jimbo la New York**

- Kuanzia Januari 1, 2025, Jimbo la New York litaanzisha Mapumziko Yaliyolipiwa kwa Akina Mama Wajawazito (Paid Prenatal Leave).
- Mkazi yeyote wa New York aliyeajiriwa katika sekta binafsi ataweza kupata masaa 20 ya nyongeza yaliyolipiwa kwa ajili ya mapumziko ya kuugua wakati wa ujauzito.
- Muda wa huduma ya afya kwa ajili ya akina mama wajawazito ni nyongeza ya muda wanaoweza kuchukua kupumzika wakiugua, na hauhitajii kulimbikizwa. Hupatikana mara tu mwajiriwa anapoanza kazi.
  - Mapumziko yaliyolipiwa ya akina mama wajawazito ni tofauti na mapumziko yanayotolewa jimboni New York kwa mtu aliye mgonjwa pamoja na aina nyingine za mapumziko au mafao.
  - Waajiri hawawezi kuwalazimisha wafanyakazi kutumia aina zingine za mapumziko kabla ya kutumia mapumziko yaliyolipiwa ya akina mama wajawazito au kuchagua aina moja ya mapumziko badala ya nyingine.
- Wafanyakazi wanaweza kutumia mapumziko ya aina hii kwa ajili ya mimba tofauti ndani ya mwaka mmoja. Hata hivyo, hawawezi kutumia zaidi ya masaa 20 ya mapumziko ya aina hii ndani ya kipindi cha wiki 52.
- Mapumziko yaliyolipiwa ya akina mama wajawazito yanawahusu wafanyakazi wote katika sekta binafsi bila kujali nafasi yao ya kazi, tasnia, ikiwa wameajiriwa kwa chini ya masaa 40 kwa wiki au ikiwa hawapati malipo ya ziada kwa kazi izidiyo masaa 40 kwa wiki.
- Huduma za akina mama wakati wa ujauzito zinahusisha pia huduma ya kupandikiza mimba pamoja na kutoa mimba.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea ny.gov/prenatal

# Shule na elimu



**Mfumo wa Shule za Umma (3K-12)**

- Jimbo la New York linahakikisha kuwa kila mtoto, bila kujali hali ya uhamiaji, ana haki ya elimu bure na yenye ubora, kuanzia elimu ya awali hadi aidha anapopokea shahada ya shule ya sekondari, au kufikia kikomo cha umri katika mwisho wa mwaka wa shule ambao mwanafunzi atatimia miaka 21.
- Familia zinahakikishiwa haki ya kupata tafsiri na huduma za ukalimani kwa hati zote zenye taarifa muhimu zinazohusu elimu ya mtoto, ndani ya muda uliopangwa.
- Wanafunzi wanaweza kutuma maombi na kujiandikisha kwenye shule za umma za Jimbo la New York wakati wowote ndani ya mwaka, ila machaguo yanaweza kuwa machache nje ya kipindi cha kawaida cha kujiandikisha.
- Shule za umma haziwezi kuulizia hali ya uhamiaji na hazitatoa taarifa za wanafunzi kwa programu yoyote ya shule ya kutwa (day school). Baadhi ya programu za watoto wadogo, zinazoendeshwa kwa masaa mengi kuliko kawaida, zinaweza kuweka kigezo cha uraia au kuangalia ukubwa wa mapato.
- Taarifa za Shule za Umma za Jiji la New York
  - Kwa taarifa kuhusu jinsi ya kuomba huduma za tafsiri ya ukalimani katika Shule ya Umma ya Jiji la New York, tembelea schools.nyc.gov/hello au piga 718-935-2013.
  - Kwa taarifa kuhusu mchakato wa ruhusa ya kuingia, tembelea schools.nyc.gov/enrollment/enrollment-help/new-students.
  - Kutafuta Shule ya Umma ya Jiji la New York na kutuma maombi ya udahili, piga 311, au tembelea Kituo cha Kukaribisha Familia (Family Welcome Center) kwa msaada. Mahali pa Vituo vya Kukaribisha Familia panapatikana katika schools.nyc.gov/fwc.
  - Vipindi cha kujiandikisha vinatofautiana kutegemea darasa/kidato. Kuona Ratiba ya Udahili kwa Msimu wa Fall 2024 (Fall 2024 Admissions Timeline), tembelea schools.nyc.gov/enroll.

**Kupigwa Marufuku kwa Simu za Mikononi katika Shule za Umma**

- Jimbo la New York lilipitisha sheria mpya Mei 2025 inayowekea kikomo matumizi ya simu za mikononi aina 'smartphone' na vyombo vingine vyenye intaneti kwa wanafunzi, wakati wa kuwepo shuleni.
- Wanafunzi wanaweza kuruhusiwa kutumia simu au vyombo vyao vyenye intaneti ikiwa vinahitajika kwa ajili ya tafsiri, fasiri, matumizi ya kitabibu, au dhurura za kifamilia
- Wazazi bado watakuwa na njia ya kuwasiliana na wanao wakiwa shuleni kupitia watumishi wa shule.
- Sheria itatekelezwa na kila wilaya ya shule kufuatana na mahitaji ya hapo karibu na mrejesho kutoka familia.
  - Shule za Umma za New York City (NYC) zitalazimu wanafunzi waweke simu zao kwenye stoo wakiwa shuleni.

**Msaada wa Kifedha wa Chuo**

- Pata msaada kutoka UnderstandingFAFSA.org, tovuti inayotoa mwongozo na taarifa mbalimbali kwa wanafunzi na familia zinazotafuta msaada wa kifedha kwa ajili ya chuo.
  - Mwongozo wa FAFSA kwa wanafunzi wa sekondari unapatikana katika lugha kumi.
  - Tovuti yao imeainisha kurasa zinazoonesha jinsi ya kukamilisha taratibu mbalimbali kwa wanafunzi wasio na vibali vya makazi pamoja na familia za wahamiaji
- Programu za msaada wa kifedha katika Jimbo la New York
  - Msaada wa kulipa ada (TAP) unawasaidia wakazi wa New York wanaokidhi vigezo kulipa ada katika shule zilizoidhinishwa katika jimbo la New York.
    - Kwa mwaka, msaada wa TAP unaweza kufikia $5,665. Kwa kuwa TAP ni ruzuku, si lazima kuirudisha.
    - Kwa taarifa zaidi au ili kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/tap
  - Udhamini wa Excelsior
    - Udhamini wa Excelsior, pamoja na programu zingine za msaada wa kifedha kwa wanafunzi, unawaweesha wanafunzi kusoma vyuo vya SUNY au CUNY bila kulipa ada.
    - Wanafunzi ambao familia zao zina mapato ya mwaka ya $125,000 au chini ya hapo wanakidhi kigezo cha kutuma maombi.
    - Kwa taarifa zaidi au kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/excelsior
  - Sheria ya DREAM ya Seneta José Peralta ya Jimbo la New York inawapa wanafunzi wasio na vibali vya makazi pamoja na wanafunzi wengine, fursa ya kupata ruzuku zinazotolewa na NYS au ufadhili wa masomo kwa ajili ya kulipia gharama za elimu ya juu.
    - Kwa taarifa zaidi au kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/dream

# Uwezeshwaji wa Kiuchumi



**Nyongeza ya Kiasi cha Manufaa ya Bima ya Kukosa Ajira**

- Mwaka huu, Jimbo la New York linaongeza manufaa ya bima ya kukosa ajira na kupunguza kodi kwa biashara.
- Kuanzia Oktoba 6, 2025, kikomo cha juu cha kiasi cha manufaa kitaongezeka kutoka $504 kwa wiki hadi $869 kwa wiki. Manufaa haya ni kwa wafanyakazi waliopoteza ajira kwa makosa yasiyo yao, ambao wako tayari kufanya kazi, na kutaka na kuweza kufanya kazi vilevile.
  - Kiasi cha manufaa cha kikomo cha juu ni kiasi kikubwa zaidi kupita vyote vingine kinachopatikana kwa wakazi wa New York wanaokosa ajira, na kinategemea mapato yaliyopita.
  - Hata kama hupati kile kiasi cha juu kabisa, inawezekana kwamba utaona nyongeza ya kiasi chako cha manufaa.
  - Kiasi kipya kitakokotolewa chenyewe kufuatana na mapato yako ya jumla yaliyoripotiwa awali.
  - Nyongeza ya kiasi cha manufaa itaanza wiki ya Oktoba 13. Hakuna kitu unachohitaji kufanya ili upokee hii nyongeza.
- Kupata makadirio ya manufaa yako ya kila wiki ya bima ya kukosa ajira, tembelea ux.labor.ny.gov/benefit-rate-calculator
- Kwa taarifa zaidi, tembelea dol.ny.gov/unemployment-insurance-ui-trust-fund-faq
- Kutuma maombi ya manufaa ya bima ya kukosa ajira, tembelea dol.ny.gov/unemployment

**Cheki za Kurudishiwa Pesa kwa sababu ya Kupanda kwa Gharama za Maisha (Inflation Refund Checks)**

- Kwa mara ya kwanza, wakazi wa New York watapata cheki za kurudishiwa pesa kwa sababu ya kupanda kwa gharama za maisha.
- Malipo haya ya kutokea wakati mmoja tu ni kwa wakazi wa New York ambao wamelipa kodi nyingi ya mauzo, kwa sababu ya kupanda kwa gharama za maisha.
- Kustahili kupata cheki ya inflation refund, sharti:
  - Umewasilisha Form IT-201, yaani fomu ya Kulipa Kodi ya Mapato kwa Mkazi wa New York, kwa mwaka wa kodi 2023.
  - Umeripoti mapato ambayo yanakidhi vigezo.
    - Kugundua kama mapato yako yanakidhi vigezo, tembelea tax.ny.gov/pit/inflation-refund-checks.htm
  - Usitajwe kama mtegemezi (dependent) kwenye fomu ya kodi ya mlipa kodi mwingine.
- Ikiwa unastahili, cheki itakutumiwa yenyewe na huhitaji kufanya kitu chochote.
  - Cheki zitaanza kutumwa kwa njia ya posta mwishoni mwa Septemba 2025, na zitaendelea kutumwa kwa wiki kadhaa.
  - Cheki zitatumiwa anuani yako uliyotumia kwenye fomu ya kodi uliyowasilisha karibuni zaidi.
  - Hakuna uwezo wa kuchagua direct deposit (kuingiziwa pesa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki) kama njia ipendelewayo.
- Kuwa mwangalifu kuhusu utapeli
  - Idara ya Kodi na Fedha ya Jimbo la New York haitawasiliana na walipa kodi kuhusu cheki za inflation refund.
  - Huhitaji kutoa taarifa zaidi kupokea cheki.
  - Ikiwa mtu anayedai kuwa anafanya kazi Idara ya Kodi anawasiliana nawe kuhusu cheki ya inflation refund, uiripoti mara moja.
- Kwa taarifa zaidi, tembelea tax.ny.gov/pit/inflation-refund-checks.htm

**Taarifa kwa Walipa Kodi Wanaofaili kutumia ITIN (Individual Taxpayer Identification Number, au Namba ya Kutambulisha Mlipa Kodi Binafsi)**

- Aprili 2025, Mamlaka ya Mapato (Internal Revenue Service [IRS]) ilifanya makubaliano na Wizara ya Usalama wa Ndani (Department of Homeland Security) kushirikishana taarifa na data muhimu kuhusu walipa kodi wasio na vibali vya makazi ambao wamepewa amri za kuondolewa nchini.
- Kwa taarifa zaidi kuhusu ITINs na faragha ya data, tembelea nyic.org/resources-training/taxpayer-information-for-itin-filers

# Demokrasia

**Uchaguzi Mkuu wa Serikali ya Shirikisho, Jimbo, na Mitaa**

- Siku ya Uchaguzi Mkuu kwa chaguzi za serikali ya shirikisho, jimbo, na mitaa ni Novemba 4, 2025.
- Siku ya mwisho kujiandikisha kupiga kura katika uchaguzi huu mkuu, au kubadilisha anuani, ni Oktoba 25, 2025.
- Kupitia usajili wako wa kupiga kura, na ushirikishaji wako wa chama, tembelea voterlookup.elections.ny.gov.
    - Ikiwa una maswali kuhusu hali yako ya usajili, wasiliana na Bodi ya Uchaguzi ya wilaya yako (county Board of Elections): www.elections.ny.gov/CountyBoards.html
    - Wakazi wa NYT: tembelea vote.nyc
- Kipindi cha kupiga kura mapema kwa uchaguzi mkuu ni kuanzia Oktoba 25 hadi Novemba 2.
- Siku ya mwisho ya kuomba kupiga kura kwa njia ya barua ni Oktoba 25. Lazima barua yenye kura ipigwe mhuri Novemba 4 au kabla, na kupokelewa na bodi ya chaguzi Novemba 11 au kabla.
    - Kutuma maombi ya kupiga kura kwa njia ya barua, tembelea elections.ny.gov/request-ballot
- Kwa uchaguzi wa 2025, wakazi wa New York watakuwa wanawapigia kura meya, madiwani wa jiji, na maafisa wengine wa mitaa na mahakamani.
- Pia, wapiga kura wa New York City watapigia kura mapendekezo ya kura kuhusu makazi na chaguzi za mitaa. Kupata taarifa zaidi, tembelea nycvotes.org




**Haki zako katika Kituo cha Kupiga Kura**

- Wapiga kura wanaweza kutumia kituo CHOCHOTE cha kupiga kura katika kaunti wanayoishi, isipokuwa New York City, ambapo kila mpiga kura ameadikishwa kwa anuani kupiga kura sehemu moja tu.
- Iwapo unadhani kuwa unastahili kupiga kura na umejiandikisha kwa wakati, lakini jina lako halijaonekana kwenye orodha ya wapiga kura, unaweza kuomba kupiga kura kwa kutumia kura ya muda (provisional ballot) au kura ya afidaviti (affidavit ballot).
- Huhitaji kuonesha kitambulisho wakati wa kupiga kura hata kama ni mara yako ya kwanza kupiga kura.
- Unaweza kupiga kura hata kama huna makazi maalumu ya kuishi.
- Katika mazingira fulani, unaweza kupiga kura hata kama umewahi kuhukumiwa kwa kosa kubwa la uhalifu.
- Kufahamu zaidi nani anaweza kupiga kura: www.nycvotes.org/how-to-vote/voting-rights
- Baadhi ya wafanyakazi wa Jimbo la New York wanaweza kupewa hadi masaa mawili ndani ya muda wa kazi bila kuathiri malipo yao ili wakapige kura. Angalia kama unastahili: www.elections.ny.gov/NYSBOE/elections/TimeOffToVoteFAQ.pdf

**Jiandikishe kupiga kura**

- Unaweza kujiandikisha kupiga kura iwapo una miaka 16+, raia wa Marekani na mkazi wa NY kwa angalau siku 30 kabla ya siku ya uchaguzi.
    - Ikiwa una umri wa miaka 16 au 17, unaweza kujiandikisha mapema lakini huwezi kupiga kura mpaka ufike miaka 18.
    - Huwezi kujiandikisha kupiga kura ukiwa jela kwa kosa la uhalifu au ikiwa mahakama imeamua kuwa huna uwezo kutokana na kuwa na ugonjwa wa akilii.
- Bodi ya Uchaguzi ya NYS: elections.ny.gov/VotingRegister.html
- Bodi ya Uchaguzi ya NYC: vote.nyc/page/register-vote
- Jiandikishe mtandaoni (ikiwa una leseni ya udereva ya NYS, Kibali au Kitambulisho Kisicho cha Udereva) : voterreg.dmv.ny.gov/MotorVoter
- Jiandikishe kwa nakala ngumu kupitia simu (Kwa Kiingereza au Kihispania): 1-800-FOR-VOTE (1-800-367-8683)
- Huna uhakika kama umejiandikisha kupiga kura? Hakikisha kwa kuangalia voterlookup.elections.ny.gov

**Kujifunza zaidi kuhusu jinsi mifumo yetu ya uchaguzi inavyofanya kazi, tazama video zetu hapa: nyic.me/civics**

# Fahamu Haki Zako



**Wanajamii na wadau wanapaswa kujua haki zao wanapokutana na wafanyakazi wa Utekelezaji wa Sheria za Uhamiaji na Forodha (ICE), Ofisi ya Udhibiti wa Mipaka (Border Patrol), au chombo kingine cha dola.**

**Ukisimamishwa na afisa uhamiaji au mtu kutoka kwa chombo kingine cha dola, kumbuka:**

- Tulia. Usikimbie. Usikatae au kumzuia afisa kukukamata, kukusimamisha n.k.
- Usidanganye au kutoa hati zilizoghushiwa.
- Una haki ya kukaa kimya. Chochote utakachosema kitaweza kutumika dhidi yako
- Afisa akiomba kukukagua au kukagua vitu ulivyonavyo, una haki ya kusema hapana.
    - Hata hivyo, hupaswi kukataa kwa kutumia nguvu
    - Polisi wanaweza kukagua mwili wako kwa kukupapasa iwapo wanahisi una silaha.
- Ikiwa wewe sio raia wa Marekani na afisa wa uhamiaji anataka kuona hati zako za uhamiaji, ni lazima umuoneshe ikiwa unavyo pamoja nawe.
- Ukisimamishwa, kutiwa nguvuni au kunyanyaswa na dola, jitahidi kupata taarifa za afisa huyo ikiwemo jina, namba, na taarifa yoyote inayomtambulisha.
- Wewe au mtu mwingine katika jamii anaweza kurekodi video au sauti ya kinachoendelea unapokutana na afisa wa chombo cha dola. Unaweza pia kuandika kilichojiri baada ya wao kuondoka.
- Ni kinyume cha sheria kwa afisa wa chombo cha dola kukusimamisha, kukukagua, kukutia nguvuni au kukurudisha nchini kwako kwa sababu ya uasili, utaifa, dini, au jinsia.

**Unaweza kutoa taarifa kuhusu tukio linalohusu maafisa wa shirikisho kwa Mradi wa Kuwalinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project – IDP).**

**IDP pia inatoa taarifa za kisheria na rufaa kwa wahamiaji waliokamatwa, kupewa tiketi, au kukutwa na hatia. Piga simu 212-725-6422 au tuma baruapepe info@immdefense.org.**

**Sehemu za Faragha**

- Nyumbani kwako pamoja na “sehemu zingine za faragha” (kama sehemu za wafanyakazi tu katika eneo lako la kazi) kuna ulinzi maalumu tofauti na sehemu zinazotumika na umma kwa ujumla. Maafisa wanaweza kuingia sehemu za faragha iwapo tu wana idhini yako au wamekuonesha hati ya mahakama (iliyowekwa saini na hakimu).

**Maeneo Yanayolindwa**

- Januari 2025, utawala wa Trump ulifuta sera ya siku nyingi iliyoelekeza maafisa wa ICE na CBP kutofanya shughuli zao za utekelezaji katika “mahali maalumu” au “mahali panapolindwa,” mifano shule, hospitali na vituo vya afya, na sehemu za abudu kama makanisa na misikiti.
- Licha ya mabadiliko haya, wakazi wa New York bado wana ulinzi fulani katika sehemu hizo maalumu na za kulindwa.
- Amri ya Mtendaji wa Jimbo la New York kutoka 2018 inakataza shughuli za utekelezaji wa uhamiaji katika majengo ya jimbo la New York kama shule za umma au hospitali, isipokuwa afisa wa ICE ana hati ya mahakama.
- Sheria ya Linda Mahakama Zetu (Protect Our Courts Act) inalinda wakazi wa New York kutoka kukamatwa katika mahakama za jimbo, jiji ni manispaa bila hati ya mahakama.
- Maafisa wa ICE na maafisa wengine hawawezi kuingia “maeneo ya faragha” bila hati ya mahakama au ruhusa ya mmiliki.

**Jihadhari na Utapeli unaowalenga Wahamiaji**

- Sheria za Uhamiaji zina mambo mengi. Kuwa mwangalifu unapojadiliana na mtu yeyote kuhusu suala lako
- Zungumza na mwanasheria tu au mwakilishi wa Department of Justice (DOJ) kwa ushauri wa kisheria kuhusu suala lako.
- Usikubali kupata msaada wa kisheria kutoka kwa ‘notario’, wakala wa safari, afisa wa kodi, afisa wa masjala, au notary. Nchini Marekani, ‘notario’ siyo mwanasheria.

**Ikiwa unahitaji msaada kuhusu kesi yako au una maswali ya jumla kuhusu uhamiaji, piga simu ya bure Ofisi ya Wamarekani Wapya 1-800-566-7636.**

# Usalama wa Jamii



**Kila mtu, bila kujali utambulisho wake au iwapo ana vibali vya makazi au la, anastahili kuwa salama kwenye jamii yake.**

### Ubaguzi na Uhalifu unaotokana na chuki

- Uhalifu wa chuki ni kosa linalosukumwa na ubaguzi kwa sababu ya uasili, rangi, utaifa, jadi, jinsia, dini, imani, umri, ulemavu au mweleko wa kijinsi.
- Jimbo la New York lina Tume Maalumu ya Kudhibiti Uhalifu wa Chuki ili kukabiliana na ongezeko la matukio yanayoripotiwa ya matishio yanayosukumwa na ubaguzi, unyanyasaji na vurugu.
- Ukishuhudia tukio au ikiwa wewe ni mhanga wa uhalifu wa chuki:
    - Toa taarifa kwa Divisheni ya Haki za Binadamu NYS. Piga simu 1-888-392-3644, tuma ujumbe mfupi "HATE" kwenda 81336, au tembelea forms.ny.gov/s3/Hate-Crime-Tips. Tembelea dhr.ny.gov kwa taarifa zaidi.
    - Kuripoti uhalifu wa chuki ukiwa unatokea au hali yoyote ya hatari, piga 911 haraka.
- Uhalifu wa chuki ukiripotiwa, taarifa zote kuhusu uliyopitia, utambulisho wako na wa wengine unabaki kuwa siri.
- Unaweza kutoa taarifa kuhusu uhalifu wa chuki na kupewa huduma bila kujali iwapo una vibali vya makazi au la.

### Rasilimali za Kijamii

- Ofisi ya Kuzuia Uhalifu wa Chuki ya Jiji la New York inatoa huduma, taarifa , na msaada kwa wanajamii na mashirika mbalimbali. Taarifa zinapatikana katika lugha mbalimbali. Kwa taarifa zaidi, tembelea nyc.gov/stophate
- Kituo cha Kutoa Elimu ya Kuzuia na Kupambana na Vurugu kinafanya kazi ya kuzuia, kupambana na kuponya jamii ya New York na uhalifu wa chuki. Wana programu za elimu ya kujilinda, warsha zinazowalenga washuhudiaji, na kuwawezesha vijana. Piga 1-718-788-1775 au tembelea caeny.org kwa taarifa zaidi.

### Mitandao ya Kijamii Unayoweza kujiunga

- AAPI
    - Asian Americans for Equality: 212-979-8381, aafe.org
    - Chhaya for South-Asian and Indo-Caribbean communities: 718-478-3848, chhayacdc.org
    - Korean Family Service Center: 718-460-3800, kafsc.org
    - MinKwon Center for Community Action: 718-460-5600, minkwon.org
    - National Federation of Filipino American Associations New York: 212-684-0542, naffaa.org
    - Sikh Coalition: 516-930-0302, sikhcoalition.org
- Waafrica
    - African Communities Together: 347-746-2281, africans.us
    - African Services Committee: 212-222-3882, africanservices.org
    - Sauti Yetu Center For African Women: 718-665-2486, sautiyetu.us
- Waarabu/Waislamu
    - Arab American Association of New York: 718-745-3523, arabamericanny.org
    - Council on American-Islamic Relations of New York: 646-665-7599, cair-ny.org
    - Muslim Community Network: 347-519-2755, mcnny.org
- Watu wenye ulemavu
    - Center for Disability Rights: 585-546-7510, cdrnys.org
    - Disability Rights New York: 518-432-7861, drny.org
- Hispanic/Latino
    - Hispanic Federation: 866-432-9832, hispanicfederation.org
    - Latino Commission on AIDS: 212-584-9325, latinoaids.org
    - Mixteca: 718-965-4795, mixteca.org
    - TransLatinx: 646-882-2000, translatinxnetwork.org
- LGBTQ+
    - Caribbean Equality Project: 347-709-3179, caribbeanequalityproject.org
    - Gay, Lesbian, Bisexual and Transgender Community Center: 212-620-7310, gaycenter.org
    - New York City Gay and Lesbian Anti-Violence Project: 212-714-1141, avp.org
- Native American na Alaska Native
    - American Indian Community House: 646-575-3638, aich.org
    - North American Indigenous Center of New York: 516-930-0302, naicny.org

# Taarifa zinazopatikana NYS



**Ofisi ya Upatikanaji wa Lugha ya NYS (Jimbo la New York)**

- Ofisi ya Upatikanaji wa Lugha ya NYS inasimamia upatikanaji wa huduma za lugha kwa mamilioni ya wakazi wa New York wasio na ustadi kamili wa lugha ya Kiingereza.
- Kufahamu haki zako za kupata huduma za ukalimani na tafsiri, tembelea ogs.ny.gov/know-your-rights
- Kufaili malalamiko kuhusu upatikanaji wa lugha, tembelea languageaccess.ny.gov/en-US.
- Kupokea toolkit (mkusanyiko wa zana) ya upatikanaji wa lugha, au kuomba toolkit ya ukalimani, uwasilishe hojani kwa mashirika ya utetezi survey.alchemer.com/s3/8252338/OLA-Questionnaire

**NYS Ofisi ya Wamarekani Wapya**

- Ikiwa wewe au mtu unayemfahamu anahitaji msaada wa bure wa kisheria, piga simu ya bure 1-800-566-7636. Taarifa zote zitatunzwa kwa usiri. Msaada unatolewa kwa zaidi ya lugha 200.

**NYS Kitengo cha Afya**

- Tuma maombi ya bima ya afya: piga 1-855-355-5777 au tembelea nystateofhealth.ny.gov.

**NYS Ofisi ya Afya ya Akili**

- Kwa taarifa zaidi kuhusu huduma za matibabu ya afya ya akili au kupata mhudumu wa matibabu ya afya ya akili, piga 1-800-597-8481 au tembelea omh.ny.gov.
- Huduma ya Kitaifa ya Kuzuia Kujiua: Ikiwa maisha yako au ya mtu unayemfahamu yako hatarini, piga 911. Ikiwa uko hali ya hatari au unahitaji msaada wa haraka, piga 1-800-273-8255 au tuma SMS "GOT5" kwenda 741-741.

**NYS Ofisi ya Kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia**

- Iwapo wewe au mtu mwingine aliye katika mahusiano ananyanyaswa na mtu mwingine kwa maneno, vitendo au kingono, au unyanyasaji wa aina nyingine, piga simu ya bure Ofisi ya NYS inayoshughulikia Unyanyasaji wa Kijinsia 1-800-942-6906.
- Kuzungumza na mshauri kwa njia ya mtandao, tembelea opdv.ny.gov. Inapatikana 24/7 katika lugha mbalimbali.

**NYS Kitengo cha Kazi**

- Kitengo cha Kazi kimejikita katika kulinda usalama wa wafanyakazi pamoja na afya, malipo/mishahara na mazingira mazuri za kazi.
- Kwa taarifa kuhusu sheria zinazohusu maslahi na masaa ya kazi, afya na usalama wa wafanyakazi, au kutuma malalamiko, piga 1-888-469-7365 au tembelea dol.ny.gov/safety-and-health
- Kwa msaada wa Bima ya Kukosa Ajira, piga 1-888-209-8124 au tembelea dol.ny.gov/unemployment/unemployment-insurance-assistance.

**NYS Kitengo cha Haki za Binadamu**

- Sheria ya Haki za Binadamu ya New York inakataza ubaguzi katika ajira, makazi, mikopo, elimu, na haki ya kuwepo sehemu za umma, kwa sababu ya umri, uasili, utaifa, jinsia, mwelekeo wa kijinsi, jinsi, ndoa, ulemavu, uanajeshi, na kadhalika.
- Ikiwa unahisi umebaguliwa, tuma malalamiko 1-888-392-3644 au tembelea dhr.ny.gov.

**NYS Makazi**

- Kwa msaada wa kutafuta makazi ya bei nafuu, piga 1-877-428-8844 au tembelea nyhousingsearch.gov.
- Kwa taarifa ya jinsi ya kushiriki kwenye bahati nasibu ya kupata makazi kwa bei nafuu katika jiji la New York, piga 212-863-7990 or visit housingconnect.nyc.gov.
- Kwa taarifa kuhusu haki za wapangaji kwenye Jimbo la New York, tembelea ag.ny.gov/publications/residential-tenants-rights-guide.

**Ofisi ya Huduma za Wahanga ya NYS**

- Iwapo wewe au mtu unayemfahamu ni mhanga wa uhalifu wa chuki, Ofisi ya Huduma za Wahanga ya NYS inaweza kusaidia kulipa gharama za huduma za matibabu na ushauri nasaha, malipo yaliyopotea, na msaada wa aina nyingine.
- Piga 1-800-247-8035 au tembelea ovs.ny.gov kwa taarifa zaidi.

Kusoma taarifa hii mtandaoni au kwa lugha nyingine, tembelea nyic.org/KYR or skani kodi hii:

Iwapo una swali lolote au maoni kuhusu nyenzo au taarifa ndani yake, tafadhali wasiliana na:
Bryan Lee – blee@nyic.org

Shirikisho la Wahamiaji wa New York (NYIC) ni sera jumuishi na shirika la utetezi linalowakilisha zaidi ya makundi 200 yanayotetea haki za wahamiaji na wakimbizi waliopo New York.

Tunaiona New York iliyo imara zaidi kwa sababu watu wote wanakaribishwa, wanahudumiwa kwa usawa na wanapewa nafasi ya kufikia ndoto zao. Dhima yetu ni kuwaunganisha wahamiaji, wanajamii na wadau ili wakazi wote wa New York wote waweze kustawi.

NYIC

**New York Immigration Coalition**
131 W 33rd St, Ste 610
New York, NY 10001
212 627 2227
nyic.org